BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 14 Juni, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):

Hotuba ya Kamati ya (PAC) Kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

II. MASWALI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

15. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Miezi michache iliyopita kumeripotiwa kadhia ya baadhi ya wazee wa kijiji cha Charawe kuwazuia watoto wao wasiende skuli ambapo idadi kubwa ya watoto walitii maagizo hayo.

(a) Je, kulikuwa na matatizo gani yaliyosababisha hali hiyo.

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa kutatua tatizo hilo.

(c) Je, ni viongozi gani walishiriki katika kutatua mzozo huo.

176. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Zamani katika skuli zetu kulikuwa na utaratibu wa madarasa ya Quran yaliyokuwa yakisaidia sana kuimarisha maadili ya vijana wetu wanapokuwa maskulini na katika jamii.

Je, kwanini utaratibu wa Madarasa ya Qur an umeondoshwa na mbadala wake ni nini.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

123. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Katika visiwa vya Zanzibar hasa Pemba kuna tatizo la kitoweo cha kuku wa kisasa kutokana na tatizo la kiwanda cha kutoa vifaranga vya kuku na chakula chake ambapo vitu hivi vinapatikana Tanzania Bara. Na kwa kuwa kisiwa cha Pemba pamoja na kuwa kuna wafugaji wa kuku wa kienyeji, lakini bado ipo haja ya kupata kuku wa kisasa kwa bei rahisi.

(a) Je, Serikali inalijua hilo na kama inalijua imechukua hatua gani.

(b) Je, kuna mpango wa dharura wa kuleta kiwanda cha kutoa vifaranga na chakula chake.

(c) Je, inagharimu kiasi gani kwa kiwanda cha kutoa vifaranga kitaalamu na kiwanda cha chakula.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

198. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kwa kuwa mafundi wa Mamlaka ya Maji wa Wilaya ya Micheweni wanakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi sambamba na tatizo la usafiri kutokana na uhalisia wa jiografia ya Wilaya ya Micheweni. Aidha, kuna tatizo la mabadiliko ya mishahara kwa wafanyakazi wa ZAWA ambapo Mashirika yote yameshafuata maagizo ya mabadiliko hayo ya mishahara.

(a) Je, Mamlaka ya Maji Pemba ina mpango gani na lini watawapatia vitendea kazi vipya mafundi kama vile spana za kuanzia namba 3 na kuendelea ambazo ndio muhimu kwa ajili ya kufungia viungo vya mabomba hayo.

(b) Je, ZAWA wana mpango gani wa kuwapatia vyombo vya usafiri mafundi bomba na fundi umeme wa Mamlaka wa Wilaya ya Micheweni ili waweze kufanyakazi zao kwa uhakika.

(c) Je, ni lini ZAWA watabadilisha viwango vya mishahara kwa wafanyazi hao.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

115. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) ndio lenye dhamana ya kununua karafuu Zanzibar ambayo inaongoza kwenye soko la dunia kwa ubora wake. Na kwa kuwa Shirika linahitaji kuwapatia wakulima na wachumaji vifaa vya kutunzia karafuu kama vile majamvi, kapu, pishi na nyenginezo na kuwepo kwa mashine za kusafishia karafuu na magunia.

(a) Je, pamoja na kukopesha fedha za kuchumia karafuu, kuna utaratibu gani wa kuwakopesha vitendea kazi wakulima wa karafuu ili kuhakikisha kwamba karafuu zote zinaanikwa kwenye majamvi na kupata karafuu nyingi zaidi zenye daraja la kwanza.

(b) Je, kwenye msimu huu wa uchumaji wa karafuu uliopita, Shirika lilinunua karafuu kiasi gani za daraja la kwanza.

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba karafuu zinahifadhiwa kwenye magunia badala ya utaratibu uliopo hivi sasa wa kuhifadhi karafuu kwenye mapolo ambayo hupelekea karafuu kusinyaa na kupoteza uzito na rangi yake ya asili.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

165. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kumekuwa na tatizo la kutofuata utaratibu pale gari inapoletwa kwenye meli kuingia nchini ambapo gari hiyo kuwa haina leseni wala bima lakini huruhusiwa kutembea barabarani kwenda alipo mhusika wake. Hata hivyo, baadhi ya gari hizo hupakiwa mizigo mengine mpaka wakati mwengine kushindwa kutembea kikawaida.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.

(b) Je, ni ruhusa kupakia mizigo gari inayotoka bandarini.

(c) Je, kama kutatokea ajali ambayo itasababishwa na gari inayotoka bandarini ambayo ndio kwanza inaingia nchini, nani atakuwa muhusika.

III. KAULI YA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Hotuba ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Zanzibar,
14 Juni, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.